*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 103-122*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.

# Ruwaza ya Utatu wa Sinonimu za Asili na za Mkopo katika Kiswahili

*George J. Kitundu[1] na Pendo S. Malangwa*

**Ikisiri**

Ukopaji wa maneno katika lugha husababisha lugha pokezi kuwa na msamiati changamani, yaani msamiati wa asili na wa mkopo (Kiango, 1999). Inasemekana kuwa lugha inapokuwa na maneno ya asili na ya mkopo hutokea wakati neno la asili likawa na uhusiano wa kimaana na neno moja au zaidi kutoka lugha za kigeni moja au zaidi na, hivyo, kuibua sinonimu zinazohusisha maneno ya asili na ya mkopo. Ullmann (1967) anaeleza kuwa visawe vya dhana moja katika lugha kutoka lugha mbalimbali havijakaa kivoloya, bali hufuata ruwaza fulani. Ruwaza hizo huitwa ruwaza za sinonimu. Ruwaza hizo zinaweza kuwa za uwili au utatu (Ullmann, 1967; Kreidler, 1998). Lugha ya Kiswahili imedhihirisha sifa ya kuwa na msamiati changamani kwa sababu ya kutohoa maneno mengi kutoka lugha za kigeni. Kuwapo kwa msamiati changamani katika lugha hii hapana shaka kuna sinonimu zinazojitokeza ambazo zinatengeneza ruwaza mbalimbali. Makala hii inachunguza ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Data za makala hii zimekusanywa kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) (2013), *Kamusi ya Visawe* (KV) (2014) na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (KKK) (2017) pamoja na kutoka kwa watoataarifa. Data kutoka vyanzo hivyo zimekusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa matini, usaili na hojaji na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui na kiulinganishi. Mjadala wa makala hii umeongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Vijenzi pamoja na Nadharia ya Matumizi.

## 1.0 Utangulizi

Sinonimu ni maneno yenye kuhusiana kimaana. Hali ya maneno kuwa na maana sawa au zilizokaribiana inaitwa usinonimu (Ullmann, 1967; Harris, 1973; Ndimele, 1997; TUKI, 2013; Kahigi, 2019; Chacha na Malangwa, 2019). Usinonimu katika

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Fasihi, Kitivo cha Humanitia na Sayansi za Jamii, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: george.jerald@yahoo.com

Malangwa ni Profesa Mshiriki, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: pmalangwa@yahoo.co.uk

lugha hutokana na sababu mbalimbali kama vile ukopaji (Kiango, 1999; King'ei, 2010; Khamis, 2014; Resani, 2015; Chacha na Malangwa, 2019). Ukopaji wa maneno huitajirisha lugha kimsamiati kwa sababu maneno mengi ya mkopo huongezwa katika lugha pokezi. Kutokana na ukopaji, msamiati wa lugha hugawanywa katika sehemu mbili; msamiati wa asili na ule wa mkopo kutoka lugha za kigeni (Kiango, 1999). Msamiati wa asili (wa Kiswahili) hautokani na ukopaji na katika kamusi nyingi za Kiswahili kama KKK (2017) na KKS (2019) msamiati huu hubainika kwa kukosa taarifa ya kietimolojia, jambo linaloashiria kuwa msamiati huo ni wa asili ya Kiswahili. Msamiati wa kigeni huu ni ule ambao unatokana na ukopaji wa maneno kutoka lugha za kigeni. Msamiati huu katika KKK (2017) na KKS (2019), umebainishwa kwa kuwekewa taarifa ya kietimolojia.


Maelezo ya wataalamu mbalimbali kama Ullmann (1967), Kreidler 1998; Resani (2015); Chacha na Malangwa (2019) yanaonesha kuwa lugha inapokuwa na msamiati changamani huibua sinonimu kwa sababu visawe vingi vya mkopo huongezwa juu ya maneno ya asili. Kwa hiyo, neno moja mathalani la asili huweza kuhusiana kimaana na neno lingine la mkopo kutoka lugha moja au zaidi. Sinonimu hizo hutengeneza ruwaza mbalimbali kama vile uwili au utata kutegemeana na idadi ya lugha zinazochangia maneno katika lugha kopaji. Makala hii inachunguza ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Katika uchunguzi huo, kwanza tumejadili dhana ya sinonimu na aina zake, chanzo cha sinonimu za asili na za mkopo pamoja na ruwaza za sinonimu. Pili, tumefafanua nadharia zilizoongoza utafiti huu pamoja na mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Baada ya vipengele hivyo, makala imejadili ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Mwishoni mwa makala tumetoa hitimisho la jumla.

## 2.0 Mapitio ya Kazi Tangulizi na Kiunzi cha Nadharia

Kipengele hiki kinajadili maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu pamoja na kubainisha kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu. Sehemu inayofuata inaanza kwa kupitia kazi tangulizi.

### 2.1 Dhana ya Sinonimu

Sinonimu ni maneno yenye maana zinazokaribiana au zilizo sawa (Ndimele, 1997; Cruse, 2006; Griffiths, 2006; Massamba, 2009; Matinde, 2012; Resani, 2015; TUKI, 2019). Riemer (1988), Kreidler (1998) na Cruse (2006) wanaeleza kuwa maneno huwa sinonimu katika lugha moja pale sifa za kisemantiki katika maneno hayo zinapofanana, yaani sifa hizo zinapojitokeza katika pande zote mbili za maneno yanayojenga seti ya sinonimu. Kreidler (1998) anafafanua zaidi mfanano huo wa kisemantiki kwa kutumia Kielelezo Na. 1 ambacho kinaonesha kuwapo kwa sifabia zinazojitokeza katika maneno yenye sifa ya usinonimu.




***Kielelezo Na. 1: Uhusiano wa maneno yenye sifa ya sinonimu***

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kuwa kuna mwingiliano wa vijenzi semantiki kwa maneno mawili ya *hard* na *difficult* ambapo kati ya maneno hayo kuna sifa zinazofanana. Kuwapo kwa vijenzi semantiki au sifa zinazofanana katika maneno hayo (yaani sifa ya *ugumu* inayojitokeza katika maneno yote), ndiko kunakoyafanya maneno hayo yawe visawe vya dhana moja. Kreidler (1998) anaendelea kudai kuwa kadiri sifa zinavyolingana ndivyo kiwango cha usinonimu kati ya maneno hayo kinavyozidi kuongezeka. Kwa hiyo, usinonimu katika lugha una viwango. Kuwapo kwa viwango hivyo katika sinonimu kunatupatia aina mbili za sinonimu, yaani sinonimu kamili na sinonimu zisizo kamili.

Sinonimu kamili ni zile ambazo zina kiwango kikubwa cha usawe. Sinonimu hizi huweza kutumika katika miktadha tofautitofauti bila kuathiri maana. Aina hii ya sinonimu inapotumika katika miktadha mbalimbali huwa na maana na athari ileile. Ullmann (1967) na Kahigi (2019) wanaeleza kuwa maeneo ambayo yanaweza kuwa na sinonimu kamili ni eneo la istilahi ambapo tunaweza kuwa na mifano kama *semasiolojia* na *semantiki*, *nazali/king'ong'o, sarufi-umbo/fonolojia*, *sifa/kivumishi* na *elimu-viumbe/bayolojia*. Hata hivyo, wataalamu wengi kama Lyons (1995), Ndimele (1997), Cruse (2006), Riemer (2010) na Chacha na Malangwa (2019), wanakiri kuwa sinonimu kamili katika lugha ni chache sana na zinaweza hata kuhesabika. Sababu zinazotolewa ni kuwa katika lugha ni vigumu kuwa na maneno mawili au zaidi yenye maana sawa kabisa katika miktadha yote kwa sababu maneno yana virejelewa zaidi ya kimoja. Kwa hiyo, hakuna usinonimu kamili bali wa viwango tu. Hata hivyo, ingawa wataalamu wengi wanadai kuwa hakuna sinonimu kamili lakini tunaungana na baadhi ya wataalamu kama Ullmann (1967), Resani (2015) na Kahigi (2019) waliodai kuwa sinonimu kamili zipo ingawa ni chache sana.

Sinonimu zisizo kamili ni zile ambazo zina viwango fulani tu vya mfanano wa kimaana. Sinonimu hizo huweza kubadilishana matumizi katika baadhi ya miktadha tu, na hivyo, kuwa na athari sawa katika baadhi ya miktadha lakini zikatofautiana katika miktadha mingine (Dixon, 1991; Ndimele, 1997; Riemer 2010). Riemer (2010) anafafanua zaidi hoja hii kwa kutumia mfano wa maneno *pupil* na *student.* Anadai kuwa maneno haya yanakuwa sinonimu tu kama yatahusisha muktadha wa shule au elimu kwa maana ya mtu anayefundishwa na mwalimu. Ikiwa

*pupil* itarejelea jicho basi maneno hayo si sinonimu. Hivyo, *pupil* na *student* ni moja ya mifano ya sinonimu zisizo kamili kwa sababu zinahusiana katika moja ya dhana zake tu. Kipengele kinachofuata kinafafanua chanzo cha sinonimu za asili na za mkopo.

## 2.2 Chanzo cha Sinonimu za Asili na za Mkopo

Sinonimu za asili na za mkopo hutokana na sababu kubwa ya ukopaji wa maneno katika lugha. Kiango (1999) anaeleza ukopaji wa maneno kuwa ni kitendo cha kuchukua msamiati wa lugha fulani na kisha kuutumia katika lugha nyingine. Anaendelea kueleza kuwa ukopaji wa maneno si suala la lugha fulani maalumu tu, bali ni mbinu ya kukuza lugha inayotumiwa na lugha zote duniani, Kiswahili kikiwamo. Kuna namna mbili za ukopaji wa maneno. Kwanza, kukopa kutoka lugha ambazo kiisimu ziko katika familia moja. Mathalani, lugha ya Kiswahili hukopa maneno kutoka lugha zingine za Kibantu ambazo zina mnasaba na Kiswahili. Pili, kukopa kutoka lugha za kigeni ambazo zinatofautiana kiisimu (Kiango, 1999).

Hoffer (2005) anaeleza kuwa matokeo ya wazi kutokana na kuwapo kwa mwingiliano wa tamaduni ni kuwapo kwa maneno ya mkopo katika lugha kutoka lugha mbalimbali. Anaendelea kueleza kuwa mzungumzaji wa lugha anaweza kukopa neno na kulibadilisha na kuwa na matamshi ya lugha pokezi. Pili, anaweza kuchukua kama lilivyo kutoka lugha chanzi na kulitumia katika lugha pokezi. Tatu, anaweza kubadilisha sehemu ya neno tu, yaani sehemu moja kuwa ya mkopo na nyingine kuwa ya asili. King'ei (2010) anadai kuwa lugha ya Kiingereza imekopa msamiati mwingi kutoka lugha za Kilatini, Kigiriki, Kifaransa, Kijerumani na Kiarabu. Msamiati huo hukopwa kutegemeana na mahitaji ya nyanja fulani kama vile utawala, serikali na utamaduni. Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha zingine, nayo imekopa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni (Chuwa, 1988; Besha, 1995; Chacha na Malangwa, 2019). Maneno katika lugha hayakopwi tu kiholela bali kuna sababu mbalimbali zinazochochea ukopaji huo. Baadhi ya sababu hizo zinafafanuliwa katika aya zinazofuata.

Kwanza, ukopaji wa neno hutokana na mahitaji ya msamiati katika lugha kwa ajili ya kuelezea dhana fulani. Gray (1964) na Kiango (1999) wanaeleza kuwa ukopaji wa neno hufanyika ikiwa neno linalokopwa linasimamia dhana au kitu ambacho hakikuwa kinajulikana katika jamii ya lugha hiyo. Kiango anaeleza zaidi kuwa nchini Tanzania, kabla ya kuja kwa wageni, hapakuwa na dhana zinazowakilishwa na maneno kama vile *school*, *train* na *hospital*. Hivyo, wageni walipokuja na dhana hizo, Kiswahili kilikopa maneno hayo na kuyatohoa ili yafuate mfumo wa lugha ya Kiswahili na kupata maneno kama *skuli*, *treni* na *hospitali*. Hata hivyo, ukopaji huu kwa kiasi fulani husababisha ongezeko la maneno kuliko ongezeko la visawe kwa sababu maneno hukopwa ili kuelezea dhana ambazo hazijulikani katika lugha husika. Ikiwa maneno hayo yatakopwa kutoka katika lugha mbili tofauti kama ilivyo kwa *shule* (kutoka Kijerumani) na *skuli* (kutoka Kiingereza), ndiyo yanaweza kusababisha kuwapo kwa sinonimu.

Pili, kuwapo kwa maingiliano ya nguvu kisiasa na kiuchumi husababisha ukopaji wa maneno. Jamii zinazotawaliwa hulazimika kutumia maneno ya lugha tawala, na hivyo, kuongeza msamiati katika lugha tawaliwa hata kama msamiati unaoelezea dhana hiyo ulikuwapo (Robins, 1964; Chuwa, 1988; Kiango, 1999). Mathalani, katika lugha ya Kiswahili kutokana na kutawaliwa na Waingereza na Wajerumani, jamii ambazo zina nguvu kisiasa na kiuchumi, maneno mengi yalitoholewa kutoka lugha za Kiingereza na Kijerumani kuja lugha ya Kiswahili. Hii ndiyo maana kuna jozi mbalimbali za sinonimu kama *shule*/*skuli* ambazo zinarejelea mahali wanafunzi wanapofundishwa mathalani elimu.

Tatu, ukopaji wa msamiati kutokana na kasumba ya wazungumzaji wa lugha fulani kupenda kukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali licha ya kuwapo kwa msamiati unaorejelea dhana hizo katika lugha yao (Kiango, 1999). Katika namna hii ya ukopaji, istilahi inaweza kukopwa si kwa sababu haipo katika lugha husika, bali kwa vile wenye istilahi inayokopwa wanaonekana kuwa na ustaarabu wa juu zaidi, na hivyo, kuufanya msamiati wao kuonekana kuwa bora zaidi. Kila jamii inapoingiliana na jamii zingine hukopa msamiati hata kama msamiati unaosimamia dhana hiyo upo au umekopwa kutoka lugha zingine (Zhou, 2016). Matokeo ya ukopaji huu ni ongezeko la visawe vya kigeni juu ya maneno ya asili jambo ambalo husababisha kuwe na maneno mawili au zaidi yenye maana zilizo sawa au zinazokaribiana.

Kulingana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa ukopaji unaotokana na kasumba ya watu kukopa msamiati pamoja na kutawaliwa kwa nguvu na jamii zenye nguvu kisiasa na kiuchumi ndiko kunakosababisha kuibuka kwa sinonimu zenye asili tofauti. Hii ni kwa sababu katika maingiliano ya lugha moja na nyingine, watu hukopa msamiati toka kwenye lugha hizo ingawa msamiati huo upo katika lugha yao na, hivyo, kuibua sinonimu za asili na za mkopo. Inaelezwa kuwa panapokuwapo na sinonimu za asili na za mkopo katika lugha, na Kiswahili kikiwamo, sinonimu hizo hutengeneza ruwaza mbalimbali ambazo zinaitwa ruwaza za sinonimu, dhana inayojadiliwa katika kipengele kinachofuata.

## 2.3 Ruwaza za Sinonimu

Neno ruwaza limefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalani, Massamba (2009) anaeleza kuwa ruwaza ni utaratibu wa kimpangilio wa vipashio vya lugha. TUKI (2013) kwa upande wao wanafafanua ruwaza kuwa ni mpangilio maalumu wa mambo. Mpangilio huo unahusisha uwekaji wa vitu katika mfuatano fulani kulingana na sifa au vigezo mbalimbali. Maelezo haya, tukiyahusisha na lugha yana maana kuwa maneno ya lugha hayapangwi kiholela tu, bali hufuata misingi au vigezo mbalimbali. Kwa kuzingatia maelezo hayo, dhana ya ruwaza za sinonimu inatumiwa katika utafiti huu kama mpangilio wa sinonimu kulingana na matumizi ya sinonimu hizo katika jamii. Kigezo kikuu kinachotumika katika kupanga sinonimu hizo ni matumizi yake katika jamii, yaani namna watu wanavyoyatumia au kuyafahamu

maneno hayo ambapo husababisha kuwa na neno lenye matumizi makubwa kuliko lingine huku likifuatiwa na neno lenye matumizi madogo.

Akifafanua zaidi kuhusu ruwaza za sinonimu, Ullmann (1967) anaeleza kuwa, lugha inapokuwa na maneno yenye asili tofauti husababisha kuwa na ruwaza mbalimbali za sinonimu. Ruwaza hizo huambatana na tabia mahususi. Anaendelea kudai kuwa katika lugha ya Kiingereza, ambayo ina maneno mengi ya mkopo kutoka lugha mbalimbali, sinonimu zinafuata kanuni kuu mbili: kanuni ya uwili na ya utatu. Kanuni hizi ndizo zinazotengeneza ruwaza za sinonimu. Kanuni ya uwili inahusisha sinonimu kutoka lugha mbili tofauti, kwa hivyo, kutupatia ruwaza ya uwili. Ruwaza ya uwili inahusisha neno la asili na la mkopo kutoka lugha zingine kama vile Kifaransa, Kilatini au Kigiriki (Ullmann, 1967). Kwa hiyo, kuna ruwaza ya uwili ya Kiingereza-Kifaransa/Kilatini/Kigiriki.

Kanuni ya utatu inahusisha sinonimu kutoka lugha tatu tofauti: Kiingereza (lugha ya asili)-Kifaransa-Kilatini au Kigiriki (Ullmann, 1967; Kreidler, 1998; Danglli, 2010; Chacha na Malangwa, 2019). Ullmann (1967) anatoa mfano wa visawe *end-finish-conclude* wenye maana *mwisho-maliza-hitimisha* katika Kiswahili kushadidia hoja hiyo. Katika mfano huo, neno *end* linatoka katika lugha ya asili, yaani Kiingereza, *finish* linatoka katika lugha ya Kifaransa na *conclude* linatoka katika lugha ya Kigiriki. Ullmann (1967) anaeleza kuwa maneno yanayojenga ruwaza hizo huwa na tabia mbalimbali. Mathalani, neno la asili huwa la kwanza katika ruwaza huku yale ya kigeni yakiwa ya pili au tatu. Vilevile, maneno ya asili huwa si rasmi na yenye matumizi ya kawaida ikilinganishwa na visawe vyake vya kigeni ambavyo huwa rasmi zaidi. Mathalani, yapo yanayoweza kuwa rasmi na mengine si rasmi kama ilivyo kwa *wife* au *spouse* ambayo ni rasmi huku *missus* au *old lady* yakiwa si rasmi. Hata hivyo, tabia za visawe hivyo hubadilika kulingana na ongezeko la visawe kutoka lugha mbalimbali (Ullmann, 1967; Saeed, 1997).

Ruwaza za uwili na utatu zinazojitokeza katika lugha ya Kiingereza, zinajitokeza pia katika lugha zingine kama Kifaransa ambayo nayo ina maneno ya mkopo kutoka lugha za kigeni. Hata hivyo, kuna tofauti za msingi zinazojitokeza katika ruwaza hizo (Ullmann, 1967). Vilevile, ruwaza hizo zinajitokeza pia katika lugha ya Kialbania ambayo nayo kutokana na ukopaji wa maneno ina seti kadhaa za sinonimu zinazohusisha maneno ya asili na ya mkopo ambapo memba wa seti hizo wanatoka katika lugha tatu tofauti. Lugha hizo ni pamoja na Kigiriki, Kilatini na Kiingereza (Danglli, 2010).

Sababu za kuwapo kwa ruwaza za sinonimu za asili na za mkopo katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kialbania zinatokana na lugha hizo kukopa maneno kutoka lugha mbalimbali (Ullmann, 1967; Kreidler, 1998; Danglli, 2010; Chacha na Malangwa, 2019). Mathalani, lugha ya Kiingereza, kama ilivyoelezwa hapo juu, imekopa maneno kutoka lugha za Kifaransa, Kilatini na Kigiriki wakati lugha ya Kifaransa imekopa maneno kutoka lugha kama Kiingereza, Kiitaliano, Kijerumani, Kilatini na Kigiriki (Ullmann, 1967) huku lugha ya Kialbania nayo ikikopa maneno kutoka lugha za Kigiriki, Kilatini na Kiingereza (Danglli, 2010). Ullmann (1967)

anaeleza kuwa tabia kama hiyo si ya Kiingereza na Kifaransa pekee kwani hujitokeza pia katika lugha zingine. Hata hivyo, suala la asili, namna na mawanda ya ruwaza hizo yatategemea historia ya lugha husika (Ullmann, 1967). Kwa mantiki hiyo, ruwaza zinaweza kutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kwa sababu ya kuwapo kwa tofauti za kihistoria katika lugha.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, Resani (2015) na Chacha na Malangwa (2019) wanasema kuwa hali kama hiyo (ya lugha ya Kiingereza) inaweza kujitokeza pia katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiswahili nayo ina maneno mengi ya mkopo kutoka lugha mbalimbali. Resani anathibitisha hilo kwa kutoa mfano wa sinonimu *mganga-tabibu-daktari* ambapo neno *mganga* ni la asili (asili ya Ubantu), *tabibu* lina asili ya Kiarabu na *daktari* lina asili ya Kiingereza. Pia, anatoa mfano *kidonda* (Kibantu) na *jeraha* (Kiarabu). Katika maneno hayo Resani anadai kuwa maneno yenye asili ya kigeni kama Kiingereza ni rasmi zaidi ikilinganishwa na yale ya Kiswahili asilia ambayo si rasmi. Ingawa hakuna ufafanuzi wa kutosha kuhusu suala hili kutoka kwa Resani lakini mifano yake inaashiria kuwa kuna ruwaza za uwili na utatu zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu ruwaza za sinonimu yanadokeza kuwa kila lugha yenye maneno ya asili na ya mkopo ina sinonimu. Sinonimu hizo hutengeneza ruwaza mbalimbali. Ruwaza hizo zina mienendo tofautitofauti kulingana na historia ya lugha inayohusika (Ullmann, 1967; Kreidler, 1998; Griffiths, 2006; Resani, 2015). Lugha ya Kiswahili nayo ina sifa hizo, yaani ina maneno ya asili na ya mkopo kutoka lugha mbalimbali kutokana na ukopaji (Chuwa, 1988; Kiango, 1995; King’ei, 2010; Chacha na Malangwa, 2019). Kwa mantiki hiyo, kuna ruwaza za sinonimu zinazoweza kujitokeza. Makala hii inachunguza ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo.

### 2.4 Kiunzi cha Kinadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia za Vijenzi Semantiki na Matumizi kama inavyofafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

#### 2.4.1 Nadharia ya Vijenzi Semantiki

Nadharia ya Vijenzi Semantiki iliibuka mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960 huko Ulaya na Marekani. Nadharia hii iliibuka kutokana na mawazo ya wanamuundo wa kifonolojia ambao waliitumia katika kutofautisha fonimu katika lugha, lakini kwa Ulaya iliibuka kutoka katika nadharia ya kikoa leksika wakati Marekani ilichipuka kutoka kwa wanaisimu anthropolojia kama vile Kroeber, Conklin na Lounsbury (Geeraerts, 2009). Kwa upande wa Ulaya, mawazo ya nadharia hii yanajitokeza katika kazi za Eugenio Coseriu, Bernard Pottier na Algirdas Greimas katika miaka ya 1960 (Geeraerts, 2009). Dai la msingi la nadharia hii ni kuwa leksimu zote zinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia seti siukomo ya vijenzi-semantiki ambavyo ni vya kijumla (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019). Kwa hiyo, katika nadharia hii, maana ya neno huweza kubainika kwa kuangalia vijenzi

vyake. Vijenzi hivyo vinabainishwa na Weisgerber kuwa ni jenda au koo (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019).

Kahigi (2019) anaeleza kuwa kupitia Nadharia ya Vijenzi Semantiki, leksimu *mwanamke* maana yake huweza kubainishwa kwa vijenzi au nduni jumuishi tatu: *mtu*, *mtu mzima* na *me* (Kahigi, 2019). Kijenzi semantiki *mtu* humtofautisha na viumbe ambavyo sio watu. Kijenzi *mtu mzima* humtofautisha mwanamke na msichana na kijenzi *me* humtofautisha mwanamke na mwanaume. Kwa kifupi nduni hizo huonekana kama ifuatavyo: *Mwanamke* =[+MTU], [+MTU MZIMA], [-ME]. Nadharia hii imetumika kubainisha maneno yenye kufanana kimaana kwa kuangalia mfanano wa vijenzi semantiki vyake. Kwa hiyo, maneno yenye kufanana kimaana katika vijenzi vyake vyote au baadhi ni dhahiri kuwa yana sifa za kuwa na usinonimu kamili au usio kamili.

### 2.4.2 Nadharia ya Matumizi

Nadharia ya Matumizi iliasisiwa na Wittgenstein (1953). Wittgenstein akinukuliwa na Resani (2015) anasema kuwa maana ya neno ni matumizi yake katika lugha. Anaeleza zaidi kuwa mtu hapaswi kuuliza maana ya neno bali aulize matumizi ya neno. Kwa hiyo, kila neno la lugha lina kazi yake na, hivyo, ukitaka kung'amua maana yake basi angalia namna neno hilo linavyotumika katika jamii. Nadharia hii inasisitiza kuwa maana ya maneno ya lugha inatokana na matumizi yake katika mfumo wa lugha. Neno la lugha halina maana isipokuwa linapata maana linapokuwa kwenye matumizi yake au kwenye muktadha maalumu. Kwa hiyo, katika nadharia hii muktadha unapewa nafasi kubwa katika ufasiri wa maana. Nadharia hii imetumika kubainisha namna maneno yanavyotumika katika jamii, na hivyo, kutupatia neno lenye matumizi makubwa kuliko lingine na hatimaye kupata mpangilio wa maneno hayo kimatumizi. Kipengele kinachofuata kinafafanua mbinu za utafiti. Aidha, kutokana na nadharia hii kusisitiza mabadiliko ya maana kutokana na muktadha, imeweza kuonesha namna maneno yanavyobadilika kulingana na mabadiliko ya muktadha na hatimaye kuathiri pia mfuatano wa maneno katika ruwaza.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu umekusanya data kutoka maktabani na uwandani. Sampuli ya utafiti huu imehusisha matini tatu za kamusi ambazo ni KKS (2013), KV (2014) na KKK (2017) pamoja na watoataarifa 70 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (CKMM). Sampuli ya matini na watoataarifa imetokana na mbinu mbili za usampulishaji, yaani usampulishaji kwa madhumuni maalumu ambayo ilitumika kuteua matini tatu za kamusi na usampulishaji nasibu tabakishi ambayo ilitumika kupata watoataarifa 70 kutoka matabaka manne tofauti ya ngazi za kielimu, yaani tabaka la astashahada, stashahada, shahada na la umahiri. Data za sinonimu zimekusanywa kutoka matini teule kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini na maoni ya watoataarifa huku

data zilizohusu maoni ya watoataarifa zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji na usaili. Data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa data kimaudhui na kiulinganishi (Ragin, 1987; Kombo na Tromp, 2006). Kipengele kinachofuata kinawasilisha na kuchambua data.

## 4.0 Ruwaza ya Utatu wa Sinonimu za Asili na za Mkopo

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo. Ruwaza ya utatu inahusisha maneno (katika seti moja ya sinonimu) kutoka lugha tatu tofauti. Hapa kuna neno la Kiswahili asilia na mawili ya Kiswahili yenye asili ya kigeni kutoka lugha mbili tofauti. Kwa hiyo, ruwaza hii ya utatu inakuwa na neno la Kiswahili asilia-neno la Kiswahili lenye asili ya kigeni-neno la Kiswahili lenye asili ya kigeni, yaani *Kiswahili-Kigeni-Kigeni*. Haya yanajidhihirisha kupitia data iliyokusanywa ambayo inahusisha seti za utatu 63. Kati ya seti hizo, kuna makundi madogomadogo ya ruwaza ya utatu yanayojitokeza. Makundi hayo ni pamoja na ruwaza ya utatu ya *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu*[2], *Kiswahili-Kiarabu-Kihindi*, *Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu*, *Kiswahili-Kiarabu-Kituruki*, *Kiswahili-Kiingereza-Kituruki* na *Kiswahili-Kiingereza-Kiajemi/Kireno/Kihindi*. Mfuatano wa maneno katika ruwaza hizi unatokana na maoni ya jumla ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Mfuatano huo umeelezwa kwa kila ruwaza. Ufafanuzi zaidi kuhusu makundi haya ya ruwaza ya utatu unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

## 4.1 Ruwaza ya Utatu ya Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu

Hii ni ruwaza ya utatu ambayo inahusisha seti yenye maneno matatu kutoka lugha tatu tofauti, yaani *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu*. Katika data zilizokusanywa ambazo ni seti 63, imebainika kuwa kuna seti 34 za ruwaza ya utatu zinazohusisha maneno kutoka lugha tatu. Mpangilio wa ruwaza hii, yaani *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu*, unatokana na maoni ya watoataarifa ambayo yalionesha kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiingereza yanatumika zaidi (kwa asilimia 50) kuliko maneno mengine. Maneno ya Kiswahili asilia yanafuatia kwa matumizi ambapo yanafahamika kwa asilimia 41 huku yale yenye asili ya Kiarabu, yakifahamika kwa kiasi kidogo ambapo ni kwa asilimia 9, na hivyo, yanakuwa ya tatu katika ruwaza. Jedwali Na. 1 linawasilisha kwa muhtasari data zinazohusu ruwaza ya utatu ya *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu*.

---

[2] Katika uwasilishaji na ufafanuzi wa data kwenye makala haya, majina ya lugha kama Kiingereza, Kiarabu, Kihindi, Kiajemi yanarejelea maneno ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha hizo ilhali neno Kiswahili linarejelea maneno ya asili ya Kiswahili, yaani yasiyotokana na ukopaji kutoka lugha za kigeni.

**Jedwali Na. 1: Ruwaza ya Utatu ya Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu**

| **Na.** | **Kiingereza** | **Kiswahili** | **Kiarabu** | **Kijenzi/Vijenzi Jumuishi** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Picha | Kielelezo | Taswira | Kitu halisi au mfano wake kitumiwacho kuelelezea au kuonesha kitu halisi. Alama iliyochorwa |
| 2. | Advansi | Kishanzu | Rubuni | Malipo yanayotolewa kabla ya wakati wake kuwadia au kazi kumalizika |
| 3. | Kombania | Kikosi | Afwaji | Kikundi cha watu wenye silaha |
| 4. | Ajenti | Mjumbe | Wakala | Mtu anayemwakilisha mtu mwingine katika shughuli fulani |
| 5. | Maksi | Tuzo | Alama | Alama apatazo mtahiniwa |
| 6. | Tuni | Lahani | Alhani | Sauti fulani ya ala ya muziki au wimbo |
| 7. | Deski | Saraka | Dawati | Meza inayotumika kwa kazi mbalimbali kama vile kuandikia na/au kuwekea vitu |
| 8. | Folio | Andiko | Waraka | Maandishi anayoandikiwa mtu kutoka kwa mtu mwingine kwa madhumuni ya kuarifu. Karatasi moja katika jalada la barua |
| 9. | Ripoti | Julisha | Arifu/taarifu/simulia | Julisha mtu habari ya jambo fulani |
| 10. | Familia | Kizazi | Ayali | Kikundi cha watu wa ukoo mmoja |
| 11. | Hosteli | Bweni | Dahalia | Nyumba ambamo wanafunzi hulala katika shule au chuo |
| 12. | Championi | Mshindi | Shujaa | Bingwa katika michezo |
| 13. | Cheni | Mnyororo | Silisili | Vikuku vya chuma vilivyoshikamana kama mkufu |
| 14. | Kesi | Mashtaka | Daawa | Mashitaka yanayosikilizwa mahakamani |
| 15. | Daktari | Mganga | Tabibu | Mtu anayefanya kazi ya kutibu wagonjwa |
| 16. | Domino | Dadu | Dhumna | Aina ya mchezo wa vipande 28 vya mbao, pembe au mpingo |
| 17. | Drili | Kwata | Taburi | Mazoezi ya kunyoosha viungo vya mwili. Mchezo wa gwaride la kiaskari |

| Na. | Kiingereza | Kiswahili | Kiarabu | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| 18. | Paradiso | Pepo | Janna | Mahali patukufu panapoaminiwa kuwa wanaofuata amri ya Mungu wataishi |
| 19. | Gauni | Rinda | Kanzu | Kanzu ya kike/vazi refu kama gauni |
| 20. | Gramafoni | Kinanda | Santuri | Chombo kinachotumiwa kutoa sauti kwa kupulizwa au kuguswa nyuzi au misumari yake |
| 21. | Ripoti | Taarifa | Habari | Maelezo ya jambo fulani lililotokea |
| 22. | Inspekta | Mkaguzi | Mdhibiti | Mtu anayechunguza na kuthibitisha kazi inakwenda sawasawa |
| 23. | Wadi | Kata | Hara | Eneo la utawala lililokubwa kuliko kijiji au mtaa na ndogo kuliko tarafa |
| 24. | Supamaketi | Dukakuu | Sokokuu | Duka kubwa ambalo husheheni bidhaa mbalimbali hasa vyakula ambapo mteja hujichagulia mwenyewe vitu anavyohitaji na kuvinunua |
| 25. | Modereta | Mpatanishi | Msuluhish i | Mtu anayesuluhisha watu au pande mbili zinazogombana |
| 26. | Saizi | Kipimo | Kadiri | Enye wastani fulani/kiasi cha kipimo cha kitu |
| 27. | Kristo | Mwokozi | Masihi | Jina la Yesu |
| 28. | Kuli | Mpakizi | Hamali | Mtu anayefanya kazi ya kupakia na kupakua mizigo bandarini au forodhani |
| 29. | Mesenja | Mjumbe | Tarishi | Mhudumu wa ofisi anayetumwa kupeleka barua au habari |
| 30. | Mtapta | Mtarijumani | Mkalimani | Mtu afatiriaye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda nyingine |
| 31. | Papi | Kidue | Kuleibu | Mtoto wa mbwa |
| 32. | Shifti | Zamu | Duru | Kipindi cha muda maalumu wa kufanya kazi ambacho wafanyakazi hupokezana |
| 33. | Stoo | Uchaga | Ghala | Jengo la kuwekea na kuhifadhia vitu kama chakula au vifaa |
| 34. | Ziro | Nunge | Sifuri | Nambari 0 isiyokuwa na idadi ikiwa peke yake |

**Chanzo:** Data za Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 1 linaonesha data ya ruwaza ya utatu inayohusisha maneno kutoka Kiswahili yenye asili ya Kiingereza, maneno ya Kiswahili asilia na maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu, hivyo, mfuatano wake ni wa Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu. Katika data hizo, maneno mengine yenye asili ya Kiingereza kama *picha, advansi, maksi, daktari, stoo, familia* na *cheni* yanafahamika zaidi kuliko visawe vyake kama *kielelezo* (Kiswahili) au *taswira* (Kiarabu), *kishanzu* (Kiswahili) au *rubuni* (Kiarabu), *tuzo* (Kiswahili) au *alama* (Kiarabu), *mganga* (Kiswahili) au *tabibu* (Kiarabu), *uchaga* (Kiswahili) au *ghala* (Kiarabu), *kizazi* (Kiswahili) au *ayali* (Kiarabu na *mnyororo* (Kiswahili) au silisili (Kiarabu). Kwa hiyo, panapokuwapo na maneno matatu yenye kuhusiana kimaana kama *daktari/mganga/tabibu,* inaonekana kuwa watu wengi hupendelea kutumia zaidi neno *daktari* kuliko *mganga* au *tabibu*. Hii ni kwa sababu neno *daktari* huhusishwa na usomi na urasmi zaidi ikilinganishwa na *mganga* ambalo huwa na hisia hasi katika jamii. Vivyo hivyo, kwa seti ya sinonimu kama *supamaketi/dukakuu/sokokuu*, inaonekana kuwa watu wengi hupendelea kutumia neno *supamaketi* kwa sababu linarejelea sehemu yenye hadhi ya juu zaidi kuliko *dukakuu* au *sokokuu*. Pia, katika seti *advansi/kishanzu/rubuni* inaonekana kuwa watu wengi hupendelea kutumia zaidi neno *advansi* kwa sababu linaonekana la kisomi zaidi kuliko visawe vyake *kishanzu* na *rubuni* ambavyo huonekana vya kawaida sana. Mwisho, kwa seti *stoo/uchaga/ghala,* watu wengi hupendelea kutumia zaidi *stoo* kwa kuwa linahusishwa na hadhi ya juu kuliko *uchaga* na *ghala* ambalo huonekana lenye matumizi ya kawaidia.

Hata hivyo, pamoja na maoni hayo kutoka kwa watoataarifa kuwa maneno yenye asili ya Kiingereza yanatumika zaidi kuliko visawe vyake kutoka Kiswahili asilia na Kiarabu, upo uwezekano kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili asilia au Kiarabu kufahamika zaidi kwa watumiaji kuliko yale yenye asili ya Kiingereza ingawa hii pia hutokana na mabadiliko ya muktadha wa kimatumizi wa sinonimu hizo. Mathalani, maneno ya Kiswahili asilia kama *julisha, mshindi, kinanda, mkaguzi, kata* na *mjumbe* hufahamika zaidi kuliko visawe vyake kutoka Kiingereza na Kiarabu. Vivyo hivyo, kwa baadhi ya maneno yenye asili ya Kiarabu, yapo yanayoweza kufahamika zaidi kuliko yale ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano, maneno kama *kanzu, mkalimani, dawati* na *waraka* hufahamika kuliko visawe vyake kutoka Kiswahili asilia au Kiingereza. Pia, neno *ghala* au *uchaga* huhusishwa na matumizi katika muktadha wa vijijini zaidi ikilinganishwa na stoo. Kwa hiyo, pamoja na kuwa maneno mengi ya Kiingereza yanafahamika zaidi kwa watumiaji kuliko yale ya Kiswahili asilia na ya Kiarabu, hali hiyo hubadilika kulingana na muktadha wa kimatumizi pamoja na mtazamo wa watumiaji wa maneno hayo.

### 4.2 Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiarabu-Kihindi

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu inayohusisha maneno matatu kutoka lugha tatu za Kiswahili-Kiarabu-Kihindi. Katika seti 63 za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya utatu, kuna seti 8 zinazohusisha ruwaza ya utatu ya Kiswahili-Kiarabu-Kihindi. Katika ruwaza hii, neno la kwanza ni la Kiswahili asilia kwa sababu ndilo

linalotumika zaidi. Kwa hiyo, neno hilo linakuwa mwanzoni mwa ruwaza. Neno la pili ni la Kiswahili lenye asili ya Kiarabu na neno la tatu ni lenye asili ya Kihindi. Mifano ya ruwaza hii inaoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiarabu-Kihindi**

| Na. | Kiswahili | Kiarabu | Kihindi | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kamwe | Abadani | Bilikuli | Hata kidogo |
| 2. | Andaa | Adidi | Tayarisha | Weka tayari |
| 3. | Polepole | Taratibu | Asteaste | Kwa taratibu |
| 4. | Ganja | Kasumba | Bangi | Kileo kinachotokana na mimea kama bangi. Kileo kama bangi |
| 5. | Nguli | Shujaa | Jagina | Mtu mwenye moyo thabiti mwenye uwezo wa kukabili mambo hata kama ni ya hatari |
| 6. | Hongo | Rushwa | Chai | Malipo au zawadi anayotoa mtu ili kupata haki |
| 7. | Tele | Mzo | Chakari | Zaidi ya kawaida; kupindukia/mpaka juu |
| 8. | Mbwembwe | Fahari | Madaha | Matendo na mwenendo wa kupendeza |

**Chanzo:** Data ya Uwandani na Maktabani (2020)

Jedwali Na. 2 linaonesha ruwaza ya utatu ya Kiswahili-Kiarabu-Kihindi. Katika ruwaza hii, tunaona kuwa maneno ya mwanzo, ambayo ni ya Kiswahili asilia kama *kamwe, andaa, polepole, tele* na *mbwembwe* ndiyo yanayosemekana kutumika zaidi kuliko yale ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu kama *abadani, adidi, taratibu, mzo* na *fahari* na maneno yenye asili ya Kihindi kama *bilikuli, tayarisha, asteaste* na *madaha*. Kwa hiyo, panapokuwapo na maneno kama *kamwe/abadani/bilikuli,* watu wengi hutumia zaidi neno *kamwe* kwa minajili ya kukanusha jambo fulani. Vivyo hivyo, kwa maneno kama *andaa/adidi/tayarisha,* watu wengi hutumia zaidi neno *andaa* kwa maana ya kuweka tayari kuliko neno *adidi* na kwa kiasi fulani *tayarisha* hutumika. Kwa upande wa seti *hongo/rushwa/chai*, neno *hongo* hutumika zaidi kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno kuliko kisawe chake *rushwa* ambacho hudhihirisha hisia kali zaidi. Pia, seti *ganja/bangi/kasumba,* neno *ganja* hutumiwa na watu wengi kwa sababu hupunguza ukali wa maneno au kuficha ukweli wa jambo ikilinganishwa na matumizi ya neno *bangi* ambalo liko wazi na lenye hisia kali zaidi.

Hata hivyo, ingawa maoni yanaonesha kuwa maneno mengi ya Kiswahili asilia yanafahamika zaidi lakini hii ni kwa maneno machache tu kwa sababu yapo baadhi ya maneno yenye asili ya kigeni kutoka Kihindi kama *chakari, chai, bangi* na *tayarisha* na yale ya kutoka Kiarabu kama *rushwa, fahari* na *taratibu* nayo yanafahamika pia katika baadhi ya miktadha kwenye jamii. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame ruwaza nyingine ya utatu.

### 4.3 Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu inayohusisha maneno ya Kiswahili asilia, yenye asili ya Kiajemi na yale yenye asili ya Kiarabu. Hii inajidhihirisha kupitia seti 63 za ruwaza za utatu zilizobainishwa ambapo kuna seti 13 zinazohusisha ruwaza ya

utatu ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu. Katika ruwaza hii neno la kwanza ni la Kiswahili asilia kwa sababu ndilo linalosemekana kutumika zaidi kuliko yale yenye asili ya Kiajemi na Kihindi. Maneno yenye asili ya Kiajemi yanafuatia kimatumizi huku yale yenye asili ya Kiarabu yakiwa ya mwisho katika ruwaza kwa sababu ya kutotumika sana. Kwa mantiki hiyo, ruwaza hii inakuwa ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu. Jedwali Na. 3 linawasilisha kwa muhtasari data za ruwaza ya utatu ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu.

**Jedwali Na. 3: Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu**

| Na. | Kiswahili | Kiajemi | Kiarabu | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Vizuri | Barabara | Sawasawa | Kama inavyotakiwa: sawasawa |
| 2. | Kisia | Bahatisha | Kadiria | Jaribu kupata jambo bila ya kujua matokeo yake |
| 3. | Kohozi | Gole | Balagham u | Mate kama makohozi yasiyokwisha na yanayokuwako kwenye koo la mtu |
| 4. | Patasi | Balari | Juba | Aina ya patasi |
| 5. | Kizimbwi | Bandari | Forodha | Mahali pa kutia nanga |
| 6. | Bi | Bibi | Siti | Jina la heshima kwa mwanamke ambalo hutanguliwa kabla ya jina lake |
| 7. | Ushungi | Dusumali | Utaji | Kitambaa kivaliwacho na wanawake kwa kufunika kichwa |
| 8. | Mtumbwi | Hori | Dau | Chombo cha baharini kilicho kidogo kuliko dau kinachotumika kwa kazi mbalimbali kama vile uvuvi au usafiri |
| 9. | Hanzua | Tari | Shela | Ngoma ya Uswahilini inayochezwa na wanaume kwa bakora na panga |
| 10. | Ganzi | Kibibi | Kiharusi | Hali ya kufa ganzi sehemu fulani ya mwili kwa muda fulani |
| 11. | Upo | Sila | Dila | Chombo cha kukumbia maji katika mtumbwi au mashua |
| 12. | Pumbu | Korodani | Hasua | Mojawapo ya kokwa mbili zilizo chini ya uume |
| 13. | Ufundi | Ustadi | Uhodari | Hali ya kuwa stadi/uhodari wa jambo au mambo |

**Chanzo:** Data za Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 3 linawasilisha data inayohusu ruwaza ya utatu ya Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu. Katika ruwaza hii, maneno ya Kiswahili asilia yako mwanzoni mwa ruwaza kwa sababu mengi yake ndiyo yanayosemekana kutumika zaidi katika jamii yakilinganishwa na yale ya Kiajemi na ya Kiarabu. Mathalani, maneno kama *vizuri, kohozi, patasi, ushungi, mtumbwi, ganzi* na *pumbu*, yanasemekana kufahamika zaidi kuliko visawe vyake kutoka Kiajemi na Kiarabu kama *barabara/sawasawa, gole/balaghamu, balari/juba, dusumali/utaji, hori/dau, kibibi/kiharusi* na *korodani/hasua.* Kwa hiyo, panapokuwapo na maneno matatu kutoka Kiswahili-Kiajemi-Kihindi, kama *ushungi/dusumali/utaji* au *kohozi/gole/balaghamu,* inaonekana kuwa watu wengi hutumia maneno *ushungi* na *kohozi* kuliko visawe vingine. Maneno hayo yamezoeleka kwa watumiaji wa kila siku. Hata hivyo, suala hili si kwa maneno yote bali kuna baadhi ya maneno ya kigeni kama *bandari* kutoka

Kiajemi na *shela* na *kiharusi* kutoka Kiarabu yanafahamika zaidi kuliko yale ya asili. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza za utatu, tutazame aina nyingine ya ruwaza.

### 4.4 Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiarabu-Kituruki

Hii ni ruwaza ambayo inahusisha maneno matatu; moja likiwa la Kiswahili asilia, likifuatiwa na lenye asili ya Kiarabu na la mwisho lenye asili ya Kituruki. Ruwaza hii ina seti 3 tu kati ya seti 63 zinazohusisha ruwaza ya utatu. Katika ruwaza hii, maoni ya watoataarifa yanaonesha kuwa maneno ya Kiswahili asilia ndiyo yanayofahamika zaidi kwa watumiaji kuliko yale yenye asili ya Kiarabu na Kituruki kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Ruwaza ya Kiswahili-Kiarabu-Kituruki**

| Na. | Kiswahili | Kiarabu | Kituruki | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mlawiti | Mfiraji | Afande | Mwanamume mwenye kulawiti watu wengine |
| 2. | Kanuni | Taratibu | Desturi | Taratibu au kanuni ambazo hazina budi kufuatwa |
| 3. | Kundi | Umati | Tapo | Kundi au fungu la watu |

**Chanzo:** Data za Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 4 linaonesha seti 3 za ruwaza ya utatu ambayo inahusisha maneno kutoka lugha tatu tofauti. Katika data hizo, neno *mlawiti, kanuni* na *kundi* yanasemekana kufahamika zaidi kuliko visawe vyake kama *mfiraji/afande, taratibu/desturi* na *umati/tapo.* Kwa hiyo, panapokuwapo na sinonimu *mlawiti/mfiraji/afande*, ingawa zinahusiana katika dhana ya mwanamume mwenye kulawiti wengine, hata hivyo, inaonekana kuwa watu wengi hutumia neno *mlawiti* kwa kuwa linapunguza ukali kimatumizi ikilinganishwa na kisawe chake *mfiraji* kutoka Kiarabu. Vivyo hivyo, kwa seti *kanuni/taratibu/desturi*, inaoonekana kuwa watu hupendelea kutumia zaidi neno *kanuni* kuliko desturi au taratibu. Mwisho, katika seti *kundi/umati/tapo*, licha ya kuhusiana katika dhana ya mkusanyiko wa watu eneo fulani, hata hivyo, inaonekana kuwa watu wengi hupendelea kutumia zaidi neno *kundi* kuliko *umati* kwa sababu neno *umati* hutumika kurejelea kundi kubwa sana la watu, na,hivyo, utumikaji wake ni wa mara chache ikilinganishwa na kisawe chake *kundi*. Neno *tapo* halifahamiki sana kwa watumiaji walio wengi, na hivyo, halitumiki sana. Hata hivyo, kutokana na tofauti za kimuktadha kuna mabadiliko yanayotokea katika mfuatano huo wa maneno.

### 4.5 Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiingereza-Kituruki

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu inayohusisha sinonimu za Kiswahili asilia, Kiingereza na Kituruki. Ruwaza hii ina seti mbili za sinonimu za asili na za mkopo

kati ya seti zote 63 zinazohusisha ruwaza za utatu kama inavyojidhihirisha katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiingereza-Kituruki**

| Na. | Kiswahili | Kiingereza | Kituruki | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mlinzi | Gadi | Askari | Mtu ambaye kazi yake ni kuangalia usalama wa mahali fulani |
| 2. | Kiinuamgongo | Pensheni | Bahashishi | Zawadi anayopewa mtu baada ya ajira |

**Chanzo:** Data za Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 5 linaonesha seti mbili za ruwaza ya utatu zinazohusisha maneno ya Kiswahili asilia, ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na ya Kiswahili yenye asili ya Kituruki. Kati ya maneno hayo, maneno ya Kiswahili asilia, hususani *mlinzi* na *kiinuamgongo* yametajwa na watoataarifa kuwa yanafahamika zaidi ikilinganishwa na visawe vyake kutoka Kiingereza kama *gadi* na *pensheni* na vile vya Kituruki kama *askari* na *bahashishi*. Kwa hiyo, panapokuwepo na seti ya maneno yenye kuhusiana kimaana kama *mlinzi/gadi/askari*, watu wengi hupendelea kutumia *mlinzi* zaidi ingawa hii ni kwa matumizi ya kawaida katika jamii lakini katika maeneo ya jeshi ni dhahiri kuwa *askari* hutumika zaidi. Aidha, *mlinzi* ni neno lenye dhana pana zaidi kuliko *askari* ambaye naye pia ni mlinzi. Katika seti *kiinuamgongo/pensheni/bahashishi*, inaonekana kuwa watu wengi hupendelea kutumia neno *kiinuamgongo* kuliko visawe vyake. Kwa hiyo, suala la neno la pili litategemea asili ya neno husika kwani linaweza kuwa lenye asili ya Kiingereza au Kituruki.

Hata hivyo, pamoja na hitimisho hilo katika ruwaza hii, baadhi ya maneno yenye asili ya kigeni kama *pensheni* na *askari* huweza kutumika zaidi katika jamii, n hivyo, kuufanya mfuatano huu wa ruwaza kutokuwa thabiti kwa sababu huweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya muktadha wa kimatumizi. Ruwaza nyingine ya utatu inafafanuliwa katika sehemu inayofuata.

### 4.6 Ruwaza ya Utatu Kiingereza-Kiswahili-Kiajemi/Kireno/Kihindi

Hii ni ruwaza ya utatu inayohusisha maneno ya Kiswahili asilia, ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na mwisho ni maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiajemi/Kireno/Kihindi. Katika ruwaza hii maoni ya watoataarifa kama ilivyokuwa kwa baadhi ya data zenye maneno yenye asili ya Kiingereza, yanaonesha kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiingereza ndiyo yanayofahamika zaidi kuliko yale ya Kiswahili asilia au ya mkopo kutoka lugha za Kiajemi, Kireno au Kihindi. Hivyo, maneno yenye asili ya Kiingereza yanakuwa ya kwanza katika ruwaza hii huku yale ya Kiswahili asilia yakiwa ya pili na mengine kutoka lugha za Kiajemi, Kihindi na Kireno yakiwa ya tatu. Data kuhusu ruwaza hii zinaoneshwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Ruwaza ya Utatu ya Kiswahili-Kiingereza-Kiajemi/Kireno/Kihindi**

| Na. | Kiingereza | Kiswahili | Kiajemi | Kireno | Kihindi | Kijenzi/Vijenzi Jumuishi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kisi | Donea | Busu | | | Piga kisi |
| 2. | Feni | Pangaboi | | | Panka | Kifaa kinachozungushwa kwa umeme na ambacho huleta upepo |
| 3. | Boksi | Ndusi | | Kasha | | Kasha la karatasi ngumu ambalo hutumika kuhifadhia vitu |

**Chanzo:** Data za Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 6 linaonesha seti 3 za ruwaza za utatu za sinonimu za asili na za mkopo. Kati ya seti hizo, maneno ya Kiingereza ndiyo yanayokuwa ya kwanza katika ruwaza kwa sababu ndiyo yaliyobainishwa kama maneno yanayotumika zaidi kwa watumiaji walio wengi. Mathalani, maneno kama *kisi*, *feni* na *boksi* yanafahamika kwa watumiaji wengi ikilinganishwa na maneno ya Kiswahili asilia kama *donea*, *pangaboi* na *ndusi* au maneno kama *busu* (Kiajemi), *kasha* (Kireno) na *panka (*Kihindi). Pamoja na maneno mengi yenye asili ya Kiingereza kufahamika zaidi, yapo baadhi ya maneno ya kigeni pia kama *busu* yanafahamika zaidi ikilinganishwa na kisawe chake *kisi* kutoka Kiingereza. Hata hivyo, neno hili lina asili ya kigeni pia, na hivyo, bado maneno yenye asili ya kigeni yanaendelea kufahamika zaidi ikilinganishwa na yale ya Kiswahili asilia. Kulingana na maoni kuwa maneno yenye asili ya kigeni yanafahamika kwa watu wengi zaidi, ni tofauti na hoja iliyowahi kubainishwa na Ullmann (1967) ) kuwa katika lugha ya Kiingereza, maneno mengi yenye asili ya kigeni hayafahamiki kwa watumiaji walio wengi. Katika lugha hii, hoja hiyo inaelekea haina mashiko sana kwa sababu maneno mengi yenye asili ya Kiingereza yanaonekana kufahamika zaidi ikilinganishwa na yale ya Kiswahili asilia.

Kwa ujumla, kulingana na ukusanyaji na uchambuzi wa data, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu. Ruwaza hiyo inahusisha seti anuwai zenye maneno matatu kutoka lugha tatu tofauti. Kuwapo kwa ruwaza hii kunatokana na lugha hii kukopa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni ambazo ni zaidi ya 13 (TUKI, 2013). Katika ruwaza hii imebainika kuwa kuna ruwaza ndogondogo zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na ruwaza ya *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu*, *Kiswahili-Kiarabu-Kihindi ,Kiswahili-Kiajemi-Kiarabu,Kiswahili-Kiarabu-Kituruki,Kiswahili-Kiingereza-Kituruki* na *Kiswahili-Kiingereza-Kiajemi/ Kireno/ Kihindi*.

Matokeo ya jumla ya ruwaza za utatu yanaonesha kuwa maneno mengi ya Kiswahili asilia ndiyo yanayofahamika zaidi kuliko yale ya Kiswahili yenye asili ya mkopo. Hivyo, maneno haya yanakuwa ya kwanza katika ruwaza. Hata hivyo, ingawa tunahitimisha mfuatano huo wa maneno katika ruwaza hizi za utatu, lakini mfuatano huo si thabiti kwa sababu hubadilikabadilika kulingana na lugha

zinazohusika katika seti, tofauti za kimtazamo miongoni mwa watumiaji pamoja na tofauti za miktadha ya kimatumizi. Mathalani, katika muktadha rasmi zaidi kama hospitali za rufaa neno *daktari* huweza kutumika ilhali katika muktadha wa kawaida na ambao unahusishwa na tiba za asili neno *mganga* hutumika zaidi. Pia, katika seti *gauni/kanzu/rinda* neno *kanzu* hutumika zaidi katika muktadha wa dini ya Uislamu ilhali *gauni* hutumika katika muktadha wa kawaida. Vilevile, neno *hosteli* hutumika zaidi katika muktadha wa vyuo vikuu ilhali *bweni* hutumika kwa ngazi za elimu kama msingi na sekondari. Hivyo, katika baadhi ya seti kulingana na mabadiliko ya muktadha wa kimatumizi, baadhi ya maneno yenye asili ya kigeni hutumika zaidi, na kwa hiyo, huwa ya kwanza huku yale ya Kiswahili asilia yakiwa ya pili. Hii imejidhihirisha katika ruwaza za *Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu* na *Kihindi-Kiswahili-Kiajemi* ambapo kumekuwa na mabadiliko ya mfuatano wa maneno katika ruwaza hizo, na hivyo, kuwa na ruwaza tofauti na zingine. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa ruwaza hizi mbili ni vighairi katika ruwaza za utatu zilizobainika katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ruwaza nyingi zimeanza na neno la Kiswahili asilia.

Ruwaza hii ya utatu ambayo imebainika katika lugha ya Kiswahili iliwahi pia kubainishwa na wataalamu kama Ullmann (1967) na Kreidler (1988) katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa; Danglli (2010) katika lugha ya Kialbania na kudokezwa na Resani (2015) katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, ni dhahiri kuwa katika lugha zenye maneno ya asili na ya mkopo kama ilivyo kwa Kiswahili, kuna ruwaza ya utatu wa sinonimu unaojitokeza.

## 5.0 Hitimisho

Kwa ujumla, makala hii imechunguza ruwaza ya utatu wa sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Matokeo yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu ambayo inahusisha maneno kutoka lugha tatu tofauti. Katika ruwaza hiyo ya utatu kuna ruwaza ndogondogo zinazojitokeza kulingana na lugha zinazohusika katika seti ya sinonimu. Matokeo yanaonesha kuwa maneno mengi ya Kiswahili asili ndiyo yanayofahamika zaidi kwa watumiaji walio wengi kwa sababu hutumika mara kwa mara, na hivyo, kuwa ya kwanza katika ruwaza huku yale ya kigeni kama ya Kiingereza yakifuatia. Hata hivyo, kama ilivyojadiliwa katika hitimisho la mjadala wa ruwaza kuwa mfuatano huu wa maneno si thabiti kwa sababu kuna mazingira fulani ya kimatumizi maneno ya asili hufahamika na kutumika zaidi kuliko yale ya Kiswahili asilia, na hivyo, kuwa ya kwanza katika ruwaza huku yale ya Kiswahili asilia yakiwa ya pili. Hali hii inapojitokeza inaathiri mfuatano wa maneno katika ruwaza.

**Marejeleo**

Besha, R.M. (1995). Uingizaji wa Maneno ya Kigeni katika Kiswahili, katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu 1: 9-14.

Chacha, L.M. na Malangwa, P.S. (2019). *Semantiki.* Nairobi, Kampala, Dar es Salaam na Kigali: Longhorn Publishers Ltd.

Chuwa, A.R. (1988). Foreign Loan Words in Kiswahili, katika *Kiswahili*, Juzuu 55/1& 2: 163-172.

Cruse, A. (2006). *A Glossary of Semantics and Pragmatics.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Danglli, L. (2010). Origin of Synonyms and their Acquisition as Vocabulary, katika *LCPJ Publishing.* Juzuu Na. 3/2: 66-72.

Dixon, R.M.W. (1991). *A Semantic Approach to English Grammar*. New York: Oxford University Press.

Geeraerts, D. (2009). *Theories of Lexical Semantics.* New York: Oxford University Press.

Griffiths, P. (2006). *An Introduction to English and Pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Harris, R. (1973). *Synonym and Linguistic Analysis.* Toronto na Buffalo: University of Toronto Press.

Hoffer, B.L. (2005). Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity, katika *Intercultural Communication Studies,* Juzuu XIV/2: 53-72.

Kahigi, K.K. (2019). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Kiango, J.G. (1999). Matatizo ya Utohozi wa Maneno kama Mbinu ya Kukopa Istilahi katika Lugha, katika *Mulika*. Juzuu Na. 25: 1-8.

Kiango, J.G. (1995). Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili: Zoezi lenye Njia Mbalimbali, katika *Kioo cha Lugha.* Juzuu Na. 1: 46-54.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii.* Dar es Salaam: TUKI.

Kombo, D.K. na Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Afrika.

Kreidler, C.W. (1998). *Introducing English Semantics.* London: Routledge.

Lyons, J. (1995). *Linguistic Semantics: An Introduction.* Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Mohamed, M.A. na Mohamed, S.A. (2014). *Kamusi ya Visawe.* Royapettah: Rathna Offset Printers.

Ndimele, O. (1997). *Semantics and The Frontiers of Communication*. Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Ltd.

Ragin, C.C. (1987). *The Comperative Method*. Califonia: University of Califonia Press.
Resani, M. (2015). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Print Technology.
Riemer, N. (2010). *Introducing Semantics.* Cambridge: Cambridge University Press.
Robins, R.H. (1980). *General Linguistics.* London: Lonmans.
Saeed, J.I. (1997). *Semantics*, *Toleo la 2*. Blackwell: Blackwell Pubilishi Limited.
TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: OUP.
Ullmann, S. (1967). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford.
ZHOU, Li-na. (2016). Loan Words in Modern English and Their Features, katika *Sino-US English Teaching*, Juzuu 13/3: 209-2012.